



TAARIFA YA USAJILI WA MWAKA WA SHULE WA 2020-2021

Tulipoandaa usiku za maonyesho ya Shule ya Awali na Chekechea miezi kadhaa iliyopita, tulikuwa na matarajio ya usajili wa kawaida na tulikuwa pia tunatarajia kukutana na familia wengi wapya katika Kituo cha Rasilimali ya Familia wakikuja kusajili watoto wao.

Bila shaka – kwa sababu ya hali ilivyo – hatukuweza kuendelea na usajili kama tulivyokuwa tukifanya zamani. Kwa hivyo, tulifaa kufanya mpango mpya wa usajili unaoweza kufanywa katika hali yenye usalama na bora zaidi. Kwa sababu hii, usajili wa shule ya Lowell Public Schools sasa utafanywa kwenye mtandao.

Muda wa usajili kwenye mtandao kwa shule ya awali na chekechea kwa mwaka wa shule ujao wa 2020-2021 utaanza **Jumane, Mei 26**. Wanafunzi wote wanaoingia darasa za 1-12 ambao ni wageni kwa wilaya au wanaotaka kuhamia kwa shule ya Lowell Public Schools wanaweza kujisajili pia katika muda huu.

Kiunga kwa fomu usajili kwenye mtandao utaweza kupatikana kwenye tovuti ya Kituo cha Rasilimali ya Familia: www.lowell.k12.ma.us/frc. Kiunga hiki kitaweza kupatikana kutoka saa 8 asubuhi Mei 26 na fomu ya usajili utapatikana katika lugha zifuatazo kwa ziada ya Kiingereza: Kiarabu, Khmer, Kireno na Kihispania. Kwa usaidizi kwa ligha zingine, tafadhali wasiliana na Kituo cha Rasilimali ya Familia ukipitia 978-674-4321.

Usajili utashughulikiwa kutoka Jumatatu hadi Ijumaa kutoka saa 8 asubuhi hadi 4 jioni; lakini, usajili unaweza kuwasilishwa kwenye mtandao wakati wowote.

Tarehe ya mwisho ya kuweza kushiriki katika bahati nasibu ya usajili wa shule ya awali na chekechea ni **Juni 30, 2020 aduhuri**. Baada ya tarehe hii ya mwisho, wanafunzi watakojisajili kwa shule ya awali na chekechea wataongezwa kwenye orodha ya wanaongoja na hawataongezwa kwenye bahati nasibu ya usajili.

Hapa chini ni taarifa muhimu kukusaidia na shughuli ya usajili wa mtandao.

NANI ANASTAHIKI SHULE YA AWALI NA CHEKECHEA

Watoto wanaotimiza miaka 4 kufikia au kabla ya Septemba 1, 2020 wanastahiki kusajili kwa shule ya awali. Watoto wanaopokea huduma za Elimu Maalum wanastahiki kuhudhuria shule ya awali wakiwa na umri wa miaka 3.

Watoto wanaotimiza miaka 5 kufikia au kabla ya Septemba 1, 2020 wanastahiki kusajili kwa chekechea. Hata kama mtoto wako kwa sasa hajasajiliwa katika programu ya Shule ya Awali ya Lowell Public Schools bado unafaa kujisajili kwa Chekechea.

KUCHAGUA SHULE

Kabla ya kujisajili, unafaa kutambua hadi chaguo tatu za shule. Zingatia wakati wa kuanza na kufunga shule wa kila shule, pamoja na mahitaji yako ya utunzaji wa kabla na baada ya shule.

Kumbuka kwamba Lowell imegawanywa katika sehemu mbili – Sehemu ya 1 na Sehemu ya 2. Unaweza kuchagua shule katika sehemu unaoishi, au unaweza kuchagua shule yeyote katika jiji. Bonyeza hapa ili kupokea maelezo zaidi na orodha kamili ya shule katika kila sehemu: www.lowell.k12.ma.us/schoolselection

- Tafadhali kumbuka kwamba sehemu hufaa kwa wanafunzi katika madarasa K-8 pekee.
- Familia katika shule ya awali wanaweza kuchagua shule zozote tatu; ingawa sisi huunga mkono familia wa shule ya awali kuchagua shule karibu na nyumba yao kwa sababu hakuna usafirishaji kwa shule ya awali.
- Wanafunzi katika madarasa ya 9-12 huhudhuria shule ya Lowell High School. hakuna usafirishaji kwa wanafunzi wa shule ya upili.

USAJILI

Jisajili kwenye mtandao ukipitia www.lowell.k12.ma.us/frc.

Pindi unapowasilisha fomu ya usajili, utapokea baruapepe kutoka karani anayokushughulikia kutoka Kituo cha Rasilimali ya Familia akikuuliza kutuma hati zinazohitajika. Iwapo hujapokea baruapepe hii baada ya kuwasilisha fomu ya usajili tafadhali wasiliana na Kituo cha Rasilimali ya Familia ukipiga nambari hii 978-674-4321 (tafadhali hakikisha umeangalia sehemu ya spam au matangazo katika baruapepe yako iwapo hujaona baruapepe hii katika sehemu ya ujumbe mpya).

Hati zinazohitajika utakayoulizwa kuwasilisha ni: cheti cha kuzaliwa cha mtoto wako na rekodi za chanjo, matokeo (kwa wanafunzi wa chuo cha upili pekee), picha ya utambulisho wa mzazi/mlezi anayesajili mtoto, na dhibitisho la ukaazi (nakala ya risiti ya gharama ya matumizi ya sasa, mapatano ya kukodisha, au rehani).

Iwapo unaishi na mkaazi wa Lowell na huna dhibitisho la ukaazi katika jina lako, unaweza kukamilisha hati ya kiapo cha mhusika wa tatu. Tafadhali ongea na wafanyikazi wa Kituo cha Rasilimali ya Familia iwapo huna uwezo wa kutoa dhibitisho inayotosha au kama makazi yako si madhubuti.

Pindi unapowasilisha hati zote utapokea baruapepe nyingine ya kufuatilia kutoka karani anayekushughulikia kukuarifu kuhusu hali ya usajili wako.

BAHATI NASIBU YA KUCHAGUA WANAFUNZI WA SHULE YA AWALI NA CHEKECHEA

Bahati nasibu ya uchaguzi wa wanafunzi wa shule ya awali na chekechea hufanywa kwa shule yeyote tunapokuwa na familia zaidi ya nafasi tulizo nazo. Watoto wote waliosajiliwa kati ya Mei 26, 2020 na Juni 30, 2020 kabla ya aduhuri watashiriki katika bahati nasibu hii. Wakati unaojisajili huna athari yoyote na nambari ya bahati nasibu utakaopokea.

VIUNGA MUHIMU

Taarifa ya usajili wa shule ya awali: www.lowell.k12.ma.us/preschoolregistration

Taarifa ya usajili wa chekechea: www.lowell.k12.ma.us/kindergartenregistration

Taarifa ya usajili wa madarasa ya 1-12: <https://www.lowell.k12.ma.us/generalregistration>

Taarifa ya chaguo ya shule: www.lowell.k12.ma.us/schoolselection

Taarifa zaid kuhusu hati ya kiapo cha mhusika wa tatu na sera ya McKinney-Vento: www.lowell.k12.ma.us/McKinneyVento

MASWALI?

Iwapo una maswali yeyote kuhusu shughuli ya usajili, tafadhali pigia Kituo cha Rasilimali ya Familia ukipitia nambari 978-674-4321. Kwa lugha ya Khmer, unaweza pia kupigia 978-674-2073. Na kwa Kihispania, tafadhali piga 978-674-2072. Wafanyikazi wote pia wana nambari ya lugha na wanaweza kukuunganisha na mkalimani wa lugha nyinginezo.

Mipangilio ya kurahisisha yatafanyiwa kwa familia wasioweza kujisajili kwenye mtandao.

Tunatarajia kwa furaha familia mpya zinazojiunga na shule yetu!